

**KISA CHA UPANGAJI**

1. Nasimangwa mpangaji, ni wapi nikimbilie  
Kosa langu upangaji, ni nani nimlilie  
Wamsahau mpaji, yabidi nivumilie  
Kosa langu ni kupanga, kujenga sijawezea
2. Twasakama wapangaji, kupanga usiombee  
Hata uwepo ujiji, sharti wakuwekee  
Uhisabiwe na maji, kooni wakoromee  
Kosa langu ni kupanga, kujenga sijawezea
3. Hauna huo mtaji, nyumbayo ujijengee  
Machizi utabubuji, wao kwao ulizembe  
Uufagie na mji, na bado wakusemee  
Kosa langu ni kupanga, kujenga sijawezea
4. Walio wengi magwiji, mafumbo wakutolee  
Wajiona wajengaji, vikwazo wakuwekee  
Kero zao ni za miji, mimacho wakodolee  
Kosa langu ni kupanga, kujenga sijawezea
5. Utatamani kijiji, urudi ukaishie  
Japo uwe mtendaji, makazi uhamishie  
Wao kwao upondaji, na kero wazidishie  
Kosa langu ni kupanga, kujenga sijawezea
6. Upelekwe na mwenyeji, na kodi uwalipie  
Utabezwa mpangaji, yabidi uvumilie  
Wajipachika ujaji, maisha wakupangie  
Kosa langu ni kupanga, kujenga sijawezea
7. Jikoni upike uji, na nje wakuvizie  
Wakuulize mtaji, undani waujulie  
Wewe kwao mfujaji, malengo washindilie  
Kosa langu upangaji, kujenga sijawezea
8. Na huo ukandiaji, ni vipi nielezee?  
Wao kwao ni kipaji, yabidi wapalilie  
Wajifanya wajuaji, misifa wajijazie  
Kosa langu ufukara, kujenga sikuwezea

*Msanif Shaban,  
PO Box 15311,  
Dar Es Salaam,  
Tanzania*